**HOTUBA YA NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (MB), KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA PILI CHA SERIKALI MTANDAO, KUNDI LA PILI KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA CHUO CHA SAYANSI YA KOMPYUTA, HABARI NA MAWASILIANO, CHUO KIKUU CHA DODOMA – DODOMA, TAREHE 01 FEBRUARI, 2019**

---

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Dkt. Binilith Satano Mahenge;***

***Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Peter Lawrence Msoffe;***

***Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa;***

***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari;***

***Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali;***

***Watoa Mada;***

***Wageni Waalikwa;***

***Wana Habari;***

***Mabibi na Mabwana.***

***Habari za Asubuhi.***

Ninapenda kuwashukuru wote waliohusika katika kuandaa Kikao Kazi hiki muhimu na cha pili cha aina yake. Kipekee nawashukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Laurean Ndumbaro, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Francis Michael, Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao Dkt. Jabiri Bakari, pamoja na watumishi walio chini yao kwa maandalizi haya na kwa kunialika kujumuika nanyi kwa ajili ya ufunguzi.

Ninapenda kutambua mchango wa wadau mbalimbali ambao wamefanikisha Kikao Kazi hiki. Michango yenu ya hali na mali imefanikisha kufanyika kwa tukio hili la pili kwenye Utumishi wa Umma. Kipekee ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Benki ya NMB, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Tume ya Sayansi na Technolojia (COSTECH), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) ambao wamefadhili Kikao Kazi hiki. Ninawaomba muendelee kuona umuhimu wa kusaidia tena jitihada kama hizi kwa vipindi vijavyo.

Aidha, nawashukuru watoa mada wote, kwa kukubali kujumuika nasi kwa ajili ya kuchangia ujuzi, maarifa na uzoefu wao mkubwa katika masuala mbalimbali yanayohusu Serikali Mtandao. Pia, nawashukuru washiriki wengine wote kwa kukubali kuacha kazi zao nyingine muhimu ili kujumuika nasi kwenye Kikao Kazi hiki kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujenga uelewa wa pamoja na kuendeleza uhusiano katika utendaji kazi na wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao. Hivyo, tuna fursa kubwa ya kujifunza mengi miongoni mwetu kwenye eneo hili la Serikali Mtandao. **Karibuni sana.**

***Ndugu Washiriki na Wageni Waalikwa,***

Nimejulishwa kuwa Kikao Kazi hiki kimehudhuriwa na Maofisa Masuuli wa Serikali Kuu na wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji Wakuu, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi za Umma, ambao ndio watoa maamuzi kwenye Taasisi husika. Nafahamu pia kuwa, Kikao Kazi hiki kimefuatia Kikao

Kazi cha aina hii kilichofanyika kwa siku mbili zilizopita na kuwahusisha Maofisa Watendaji wakiwemo Maofisa TEHAMA, Maofisa Ununuzi, Maofisa Mawasiliano Serikalini, Maofisa Utumishi, Maofisa Utawala, Wakaguzi, Wahandisi, Wahasibu, Maofisa Mipango na Watumiaji Mifumo ya TEHAMA ambao ndiyo watekelezaji wa maamuzi mbalimbali kwenye Taasisi zao.

Matarajio yangu ni kuwa, Kikao Kazi hiki kitakuwa chachu ya kutoa msukumo mpya wa utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, ikiwemo kujenga uwezo ndani ya Serikali na Taasisi zake na kujenga ushirikiano na kuleta uelewa wa pamoja. Aidha, Kikao Kazi hiki ni moja ya mikakati ya kujenga na kuboresha uwezo pamoja na kuimarisha mawasiliano miongoni mwa wadau wa Serikali Mtandao. Pia, kubadilishana uzoefu na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA yenye tija katika kuboresha utendaji wa Taasisi za umma ili kutatua changamoto za utendaji.

***Ndugu Washiriki,***

Kikao Kazi hiki kinaongozwa na kauli mbiu isemayo (kwa tafsiri isiyo rasmi) "***Uwianishaji wa Rasilimali za TEHAMA kwa Maendeleo ya Viwanda" ("Harmonization of ICT Resources for Industrial Development").*** Kauli mbiu hii inalenga kuonesha umuhimu na nafasi ya TEHAMA, hususan uwianishaji wa rasilimali za TEHAMA na mchango wake katika wa maendeleo ya viwanda nchini. Niwaombe, kwa umuhimu wa kipekee, mijadala yenu ijikite katika kauli mbiu hii.

***Ndugu Washiriki,***

Dhana ya Serikali Mtandao na utekelezaji wake siyo mpya katika nchi yetu. Kwa ufupi, Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia za Habari na

Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za utendaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Serikali Mtandao siyo teknolojia kama inavyochukuliwa na wengi, bali ni matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi wa kila siku. Kwa muda sasa, Serikali imetambua umuhimu wa kuboresha huduma zake kwa Umma kupitia matumizi ya TEHAMA, na hivyo kuendelea kuijumuisha katika mipango yake mbalimbali. Aidha, Mipango ya Taifa ya Maendeleo ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16 – 2020/21) inatambua nafasi ya TEHAMA katika kufikia malengo ya Taifa na hivyo kusisitiza haja ya ongezeko la matumizi yake katika utendaji wa shughuli za Serikali na utoaji huduma kwa wananchi.

Pamoja na mambo mengine, Sera ya taifa ya TEHAMA ya mwaka 2003 (iliyohuishwa 2016), ilisisitiza juu ya Serikali kutumia fursa zitokanazo na TEHAMA katika kujiendesha na kutoa huduma kwa wananachi. Katika utekelezaji wa Sera hiyo, Serikali iliamua kuanza utekelezaji wa Serikali Mtandao kupitia Mkutano wa Baraza la Mawaziri Na.3/2004 wa tarehe 20 Aprili, 2004 ambapo pamoja na mambo mengine, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliagizwa kusimamia na kuratibu uanzishwaji wa Serikali Mtandao. Utekelezaji wa uamuzi huu ulifuatiwa na kuandaliwa kwa Mkakati wa Utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini (Julai, 2013), ambao ulilenga kuhakikisha kuwa uwekezaji na utumiaji wa TEHAMA katika Utumishi wa Umma unakuwa wa manufaa kwa taifa na pia kutoa mwongozo thabiti kuhusu jinsi ya kutekeleza mifumo na mipango ya Serikali Mtandao ambayo hatimaye itasaidia kuimarisha na kuharakisha utoaji wa huduma bora, kwa haraka, kwa gharama nafuu na kwa urahisi.

***Ndugu Washiriki,***

Ili kuhakikisha TEHAMA inatoa mchango chanya katika uendeshaji na usimamizi wa majukumu ya Serikali, jitihada mbalimbali zimefanyika na mafanikio yamepatikana katika maeneo ya sera, sheria, kanuni, miongozo, viwango, mikakati, usalama, miundombinu na mifumo. Naamini sote tumeona manufaa na hatua za kuridhisha katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Mafanikio mahususi yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao (*eGA*) ili kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao na pia kutoa msaada wa kiufundi, mafunzo na ushauri wa kitaalam kwa Taasisi za Umma.

ii. Kuboreshwa kwa Sera ya TEHAMA 2003 na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Serikali Mtandao, 2013 (*National e-Government Strategy*); kutungwa kwa Sheria za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, 2010 (*Electronic and Postal Communications, 2010)*, Miamala ya Kielektroniki, 2015 (*Electronic Transactions Act, 2015*); Makosa ya Mitandao, 2015 (*Cybercrimes Act, 2015*); na Sheria ya Serikali Mtandao (*e-Government Act*) ambayo ipo katika hatua za mwisho za maandalizi.

iii. Uwekezaji kwenye miundombinu ya TEHAMA, kama vile Mkongo wa Taifa (*NICTBB*), Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (*GovNet*), Vituo vya Kitaifa vya Data (*National Data Centres*), na Masafa ya Intaneti ya Serikali (*Government Internet Bandwidth*);

iv. Kusanifu, kutengeneza, kusimika na kuendesha mifumo mhimili na tumizi ya kimkakati na kisekta kama vile Mfumo wa Rasilimali Watu Serikalini (HCMIS), Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo Serikalini (GePG), Mfumo wa Uendeshaji wa Hospitali (GoT-

HOMIS), Mfumo wa Manunuzi Serikalini (e-Procurement) na Mfumo wa Uendeshaji wa Masijala Serikalini (e-Office), na

v. Kuongeza njia mbadala za kutolea huduma kwa wananchi kwa kutumia TEHAMA, zikiwemo Tovuti Kuu ya Serikali na Tovuti za Taasisi za Umma, simu za mikononi na vifaa vingine vya kielektroniki.

Kwa ujumla wake, utekelezaji wa juhudi za Serikali Mtandao umechangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha utoaji wa taarifa na huduma kwa wananchi kwa haraka, uwazi, urahisi, gharama nafuu, zinazopatikana wakati wowote na mahali popote nchini, na duniani kote.

***Ndugu Washiriki,***

Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza taasisi za umma ambazo zimefanikiwa kuboresha utendaji kazi na kutoa huduma kwa umma kwa kutumia TEHAMA. Kwa upande wa taasisi za Serikali ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa Serikali Mtandao, ni vyema zikaongeza juhudi katika matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yao. Chukueni hatua za haraka ili kuhakikisha mnatumia fursa zitokanazo na matumizi ya TEHAMA zitakazosaidia kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Shirikianeni baina yenu na pia shirikianeni na Wakala ya eGA ili tuwe na Serikali Mtandao madhubuti. Serikali itaendelea kutoa msukumo kwenye jambo hili.

***Ndugu Washiriki,***

Pamoja na mafanikio tuliyoyapata, ni vyema tukaendelea kukumbushana kwamba eneo hili bado linakabiliwa na changamoto kadhaa za kiutekelezaji, zikiwemo:

i. Kutokuwepo kwa uwiano wa kutosha kati ya taratibu za utendaji kazi Serikalini (business processes) na teknolojia inayotumika;

ii. Kutokupata thamani halisi ya fedha zinazotolewa kwenye miradi ya TEHAMA Serikalini;

iii. Kuwepo kwa mifumo isiyowasiliana au kubadilishana taarifa (*ndani ya taasisi, na kati ya taasisi na taasisi*);

iv. Urudufu wa mifumo miongoni mwa Taasisi za Serikali yenye viwango na gharama tofauti zisizo na uhalisia;

v. Utegemezi wa wakandarasi kwa kiasi kikubwa katika kushauri, kubuni, kusimamia, kuendesha na kuhifadhi mifumo ya TEHAMA ya Serikali;

vi. Uhusiano na uratibu hafifu wa shughuli za TEHAMA ndani na kati ya Taasisi za Serikali;

vii. Uhaba wa njia za kutosha za kutoa huduma za Serikali Mtandao (*service delivery channels)* ili huduma hizo ziweze kuwafikia wananchi wote hadi vijijini, na pia wenye mahitaji maalum;

viii. Idadi ndogo ya huduma na taarifa za Serikali zinazotolewa kupitia TEHAMA; na

ix. Kuongezeka kwa matishio ya usalama wa taarifa katika mifumo na Miundombinu ya TEHAMA.

***Ndugu Washiriki,***

Tunahitaji kuongeza msukumo ili kupata ufumbuzi wa changamoto hizi kama vile kuwa na sera na sheria mahsusi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao ili kuziwezesha Taasisi za Serikali kuwa na muono na malengo yanayoshabihiana katika matumizi ya TEHAMA. Vilevile, tunahitaji kuwekeza zaidi ili kuzijengea uwezo Taasisi za Umma na kupata watumishi wenye ujuzi na weledi wa kiwango kinachohitajika ili kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Aidha, Serikali imeweka msukumo mpya katika kutekeleza Serikali Mtandao kwa kusisitiza ushirikiano na matumizi ya pamoja ya rasilimali za TEHAMA miongoni mwa taasisi za umma, kutoa miongozo na viwango mbalimbali vya kufuatwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Pia, Serikali imedhamiria kuimarisha miundombinu ya TEHAMA, uratibu wa shughuli za TEHAMA na usalama wa taarifa za Serikali. Haya na mengine mengi, yana lengo la kuongeza ufanisi katika Sekta ya Umma, kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali na kupanua wigo wa upatikanaji na ubora wa huduma kwa wananchi.

Kwa nafasi zenu kama viongozi na watendaji wakuu wa taasisi, ni lazima kuweka na kutekeleza mikakati kabambe ya namna ya kuzishughulikia changamoto hizi. Nafahamu kwamba changamoto nyingine zinahitaji jitihada za muda mrefu na mtambuka, umiliki wa pamoja wa jitihada hizo, na uelewa wa pamoja kuhusu malengo ya Serikali Mtandao. Hata hivyo, kuna mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wa kila taasisi, hivyo yaanze kufanyiwa kazi haraka

ikiwemo kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, kanuni, viwango, taratibu na miongozo ya Serikali Mtandao.

***Ndugu Washiriki,***

Kwa namna ya pekee napenda kutoa msisitizo mahsusi kuhusiana na changamoto zinazohusiana na suala la usalama mitandaoni, ambalo bila kukabiliwa kikamilifu, litaathiri kwa kiasi kikubwa jitihada zilizokwishafanyika katika eneo la Serikali Mtandao. Tatizo la usalama mitandaoni linazidi kukua kadri maendeleo ya Teknolojia yanavyozidi kukua. Kwa ajili hiyo, naziagiza taasisi zote za umma kuzingatia viwango vyote vya usalama kwenye mifumo husika katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Usalama wa taarifa za Serikali liwe jambo la lazima wakati wa kubuni, kusanifu, kujenga, kusimika na kuendesha mifumo ya TEHAMA, badala ya kujenga mfumo kwanza na unapokamilika ndipo masuala ya usalama wa mifumo ya TEHAMA yanafikiriwa. Aidha, kama njia mojawapo ya kujihakikishia usalama, utengenezaji wa mifumo yetu uzingatie programu ambazo watalaam wetu wanaweza wakatambua kinachofanyika badala ya kuwa na mifumo ambayo hatujui kinachoendelea nyuma ya pazia.

***Ndugu Washiriki,***

Mafanikio yanayotarajiwa yatafikiwa iwapo kila taasisi ya Serikali itakuwa na watalaam wa kutosha na wenye weledi. Hivyo, nawataka watendaji wakuu wote wa Taasisi za Serikali kuhakikisha mnaimarisha idara na vitengo vya TEHAMA kwa kuwa na watalaam wenye weledi, vitendea kazi vya kutosha na muundo wa usimamizi unaokubalika. Pia, kutokana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea mara kwa mara, taasisi zote zihakikishe zinawajengea watumishi

wa TEHAMA uwezo wa kitalaam ili kuendana na kasi hii vinginevyo mafanikio yaliyokwishapatikana yanaweza yasiwe na tija au tusiweze kufikia malengo ya kuhakikisha TEHAMA inatusaidia katika kutekeleza majukumu yetu na kutoa huduma kwa wananchi.

***Ndugu Washiriki,***

Napenda kuwakumbusha na kuwasisitizia kuwa jukumu kubwa la Wakala ya Serikali Mtandao ni kuratibu matumizi ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma. Hivyo, ni lazima, Taasisi zote za Umma zishirikiane na Wakala kila zinapobuni na kutekeleza miradi ya TEHAMA. Hii itasaidia kuondoa urudufu wa miradi ya TEHAMA miongoni mwa taasisi za Serikali. Hatuwezi kuendelea kufanya kama tulivyofanya hapo awali kabla ya kuanzisha Wakala. Ni ukweli usiopingika kwamba hakuna sekta yoyote iliyoendelea bila kuratibiwa, kwa hiyo ni vema mkazingatia miongozo mbalimbali inayotolewa katika kutekeleza Serikali Mtandao.

Kwa upande wa Wakala ya Serikali Mtandao, natoa rai mhakikishe mnaendelea kujenga uwezo wa kutosha na kuweka utaratibu mzuri wa kuzisaidia taasisi za Umma katika matumizi ya TEHAMA na kamwe msigeuke kikwazo. Aidha, muendelee kufanya tafiti za Serikali Mtandao ambazo zitazisaidia taasisi za Umma kuboresha utoaji wa huduma. Pia, naipongeza Wakala kwa kuwa na utaratibu wa kubuni, kujenga na kusimamia miundombinu na mifumo shirikishi ya TEHAMA ambayo inasaidia utekelezaji wa Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma.

***Ndugu Washiriki,***

Kama kauli mbiu yetu inavyotuambia, maendeleo ya viwanda nchini yanategemea pamoja na mambo mengine uwezeshaji wa TEHAMA ambayo pia inasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi na kwa haraka, na kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali kama vile uanzishaji wa biashara, uombaji wa vibali mbalimbali na huduma ambazo zinahusiana na shughuli za kiuchumi za wananchi. Hivyo, mtakubaliana na mimi kwamba, iwapo utekelezaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA utawianishwa na kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa ndani ya taasisi za umma na baina ya taasisi za umma, utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao utakuwa ni kichocheo muhimu katika kufikia maendeleo ya viwanda tunayokusudia kuyapata. Hivyo, Taasisi zote za Umma zihakikishe zinazingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao iliyowekwa na inayoendelea kuwekwa ili kuhakikisha matumizi sahihi ya TEHAMA ndani ya Utumishi wa Umma.

***Ndugu Washiriki,***

Namalizia kwa kuwakumbusha kwamba utekelezaji wa Serikali Mtandao unahitaji jitihada na utashi wa pamoja wa viongozi, watendaji, wananchi na wadau wengine. Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na kimkakati ili kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA yanakuwa na tija katika kuwahudumia wananchi na kuwaondolea kero mbalimbali.

Hivyo, niwaombe mtumie siku hii ya leo ya Kikao Kazi hiki, kusikiliza kwa umakini mada mbalimbali na kushiriki kikamilifu mijadala itakayofuata kwa umakini na uwazi ili hatimaye mtoke na mapendekezo yatakayowezesha Serikali kufanya utoaji wa huduma kwa Umma kupitia TEHAMA uwe bora zaidi, wenye ufanisi, na unaokidhi matarajio ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mwisho, natarajia kuwa Kikao Kazi hiki kitakuwa chachu ya kuanza maandalizi ya Kikao Kazi kingine kwa mwaka ujao. Ni vyema kuhakikisha kuwa ubadilishanaji wetu wa uzoefu kupitia majadiliano na kuelimishana unakuwa endelevu. Na, ni muhimu kila mmoja wenu aendelee kushiriki pale mtakapotaarifiwa.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba Kikao Kazi cha Mwaka 2019 cha Serikali Mtandao, Kundi la Pili, kimefunguliwa rasmi.

***Asanteni kwa kunisikiliza.***